# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU

***Simiyu***
***18 Juni, 2025***

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameitaka Wizara ya Kilimo kusimamia kwa karibu mageuzi ya kilimo cha pamba na kuimarisha vyama vya ushirika vya pamba kwa lengo la kuongeza manufaa kwa wakulima wa zao hilo.

Rais Dkt. Samia ametoa maagizo hayo leo katika mkutano wa hadhara wa majumuisho ya ziara yake mkoani Simiyu uliofanyika katika viwanja vya stendi ya zamani, Wilaya ya Bariadi.

Aidha, Rais Dkt. Samia amesisitiza kuwa Serikali inatilia mkazo uimarishaji wa ustawi wa wakulima wa pamba kwa kuwapatia mbegu bora na kuwaunganisha na viwanda kwa njia ya mikataba ya uzalishaji.

Amesema licha ya changamoto zilizopo kwenye mfumo wa ushirika, Serikali bado inaamini kuwa ni chombo muhimu cha kumkomboa mkulima, akiitaja pamba kama zao la kimkakati litakaolendelea kusimamiwa kwa karibu na Serikali ili kumnufaisha mkulima.

Katika hatua nyingine, Rais Dkt. Samia amezitaka Halmashauri kusimamia kwa wakati marejesho ya mikopo ya asilimia 10 ya makusanyo ya ndani inayotolewa kwa vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ili iwanufaishe walengwa wengi zaidi, na ametoa wito kwa viongozi kuondoa urasimu uliopo katika mchakato wa kupata mikopo hiyo.

Akiwa katika Wilaya ya Maswa, Rais Dkt. Samia ametoa rai kwa wananchi kuchangamkia fursa zitakazotokana na maendeleo ya miundombinu, hususan ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR inayopita Mkoani Simiyu na itakayokuwa na kituo katika eneo la Malampaka, Wilaya ya Maswa.

Rais Dkt. Samia amehimiza wananchi kujipanga kuzalisha zaidi, kuongeza thamani ya mazao na kufikia masoko ya mbali kwa kutumia usafiri nafuu wa reli hiyo.

Vilevile, Rais Dkt. Samia amesisitiza dhamira ya Serikali kuendelea kushirikiana na wawekezaji katika kuongeza mitaji na kupanua viwanda na kuongeza kuwa dhamira ya Serikali ni kuona viwanda vya ndani vikiendelea kukua nchini.

Rais Dkt. Samia ameyasema hayo leo baada ya kuzindua rasmi kiwanda cha kuchambua pamba cha Shree Rajendra Agro-Industry Limited na kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Amali ya Mwamapalala kwa niaba ya shule zote 103 za sekondari za amali zinazojengwa kote nchini.

Shaaban Kissu
Naibu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu